Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu; wala msiwazuie (kuolewa) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa, isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi; na kaeni nao kwa wema ; na kama mkiwachukia, basi huenda mchukie kitu na AllahAmetia heri nyingi ndani yake. (An-Nisaa 4:20)

JUZU 82 No. 237 | SHAWAL-DHUL'Q.1444AH | JUNI 2023 | ZAHOOR 1402 HS | BEI TSH. 700/=

Maadhimisho ya Ukhalifa

yafana Mkoani Ruvuma

Na.
Maulana Sheikh Hussein Ng'amilo Sahib - (Ruvuma).

Ukhalifa wa Jumuiya ya waislam wa Ahmadiyya toka uanze ni miaka 115 sasa imefika. Sasa leo tuta angazia mambo mbalimbali yanayohusu ukhalifa. Hii ni bahati njema iliyoje sisi kuwa ndani ya neema hii ya ukhalifa na Allah ametujaalia afya njema leo tuna adhimisha na kukumbuka neema na tunahimizana ili tuendelee kuwa watiifu katika kumtii khalifa wa zama.

1 Nini maana ya Khalifa cheo chake hadhi yake na mamlaka yake

Khalifa ni neno la kiarabu lenye maana hizi kuwa **mbadala, mrithi, mwakilishi, Mtawala na kiongozi.** Lakini hasa hutumika katika istilahi za kiislam kama kiongozi wa waislam wote duniani ambaye huchukua nafasi ya Mtume aliye fika katika zama husika. Kama vile alipo Fariki Mtume Muhammad[saw] walifuata warthi wa kiti chake ambao waliitwa makhalifa kwa maana ya cheo walichopata baada ya mtume. Khalifa ni kifupi cha neno Khalifatu rasuulullah saw, lenye maana ya makamu wa Mtume saw katika Umma wa waislam.

Na hizi ndiyo istilahi za kiislam

Pia allama Baidhawii anasema kwamba"الخَلِيفَةُ مَنْ يُخْلِفُ غَيْرَه، وَيَتُوبُ مَتَابَه (تفسير بيضاوى جلد ١ صفحہ ٥٩)

Yaani khalifa ni yule anae kuja baada ya mwingine nae anakuwa Mrithi wake. [Tafsiri baidhawii Jalada la 1 ukurasa wa 59]



Pia Allama Ibni Athiir anasema kwamba"

الْخَلِيفَةُ مَن يَقُومُ مَقَامَ الذَّاهِبِ وَيُسَمَّ مَسَدَّه (النهاية جلد ١ صفحه ٣١٥

Yaani khalifa ni yule anae simama mahala pa yule aliye ondoka na kujaza nafasi iliyo achwa wazi. [Annihaayatu Jalada la 1 ukurasa wa 315]

Mamlaka ya khalifa

Mamlaka ya khalifa ni makubwa kwa sababu anamuwakilisha mtume na hupewa muongozo na Allah juu ya mambo mbalimbali anayofanya au yanayotokea na akiwa hapati jibu la haraka. Pia khalifa katika wakati Fulani anaweza kuwa na mamlaka ya kiserikali kama ilivyo kuwa kwa makhalifa wa Mtume saw kwani hata yeye Mtume alikuwa na cheo cha Utume na pia alikuwa na cheo cha Ufalme kama serikali kwa sababu aliongoza watu wote wenye dini na wasio na dini Waislam na wasio kuwa waislam, alipofariki yeye basi makhalifa wake wakarithi mamlaka hayo ya kuwa makhalifa na kuwa Wafalme.-

2 Je makhalifa walipatikana katika Islam?

Hdithi hizi zinaonyesha wazi kwamba ukhalifa ulipatikana ndani ya Islam, maana mtume saw alisema kuwa"

عَلَيْكُمْ بِسُنَّتِي وَسُنَّةِ الْخُلَفَاءِ الرَّاشِدِينَ الْمَهْدِيِّينَ « (ترمذى كتاب العلم باب الاخذ بالسنة ابو داؤد كتاب السنة باب لزوم السنة).

Enyi Waislamu! Ni wajibu wenu kufuata Sunnah zangu na sunna za makhalifa wangu waongofu.

Mtume Muhammad saw akasema tena kuwa"

الخِلَافَةُ ثَلاثُونَ عاماً ثُمَّ يَكُونُ بَعْدَ ذَلِكَ الْمُلك (٢٢٠ صفحه ٥ جلد احمد مسند)

Yaani ukhalifa uliowekwa baada yangu utadumu kwa miaka arobaini kisha kutakuwa na kipindi cha ufalme.

Uteuzi wa Mtume na Khalifa

Inafaa kutambua kwamba mifumo miwili ya Utume na ukhalifa imetoka kwa Mwenyezi Mungu

Endelea Uk wa 7..

Nidhamu ya Mpango wa Wasia

na Wajibu wa Musi

Na.
Muhammed Mw. Ussi Sahib.
(Katibu Wasia Taifa)

Nizamu nini?

-Ni utaratibu unaofaa wa kuliendea jambo kwa mafanikio.

Wasiyyat ni nini?

Ni mpango wa kiroho wa kujitolea sehemu ya Mali kwa ajili ya kueneza Islam.

Mpango huu ulianzishwa na Masih Aliyeahidiwa[ás] mwenyewe mwaka 1905 kwa amri ya Allah wakati alipoelezwa habari ya kukaribia kifo chake.

Ni mpango madhubuti wa kusaidia kuenea kwa Islam na kuimarika kwa nizamu ya Ukhalifa.

Mpango huu ni sawa kabisa na Aya ifuatayo ya Quran tukufu ***Hakika Allah amenunua kwa waaminio nafsi zao na mali zao ili wapate pepo" (Sura At-tauba 9:111)***

Mpango wa Wasiyyat ulianzaje?

Masih Aliyeahidiwa[ás] aliuanzisha



Maulana Sh. Tahir Mahmood Chaudhry Sahib. Akihutubia mara baada ya Semina ya Wasia

mpango huu kipindi cha mwisho wa uhai wake kwa lengo hili ambalo Allah alimfunulia juu ya kifo chake kwamba aandae sehemu maalumu kwa ajili ya kuzikwa yeye na pia sehemu hiyo itakuwa mahususi kuzikwa wale watu wenye Jazba kindakindaki kwa ajili ya dini ya Islam.

Eneo la sehemu hiyo ya kuzikiwa lilitajwa kwa jina la ***Bahshti Maqbara***, yaani Makaburi ya watu wa peponi

• Hivyo kwa Jazba yake Masih Aliyeahidiwa[ás] hakupenda kila mtu azikwe katika eneo hilo la ***Bahshti Maqbara***, bali aliona ni muhimu kuweka masharti fulani maalumu ili wale watakao tekeleza masharti hayo ndio wapate kuzikwa humo.

Utaratibu wa kulipa Wasiyyat

Wasiyyat hulipwa kuanzia kiwango cha 1/10 hadi 1/3. Ikimaanisha kuwa kiwango cha chini cha kutoa mali katika mpango huu wa wasiyyat ni 1/10 na kiwango cha juu ni 1/3.

Endelea Uk wa 4..

Ukinaifu ndani ya Ndoa uk. 03..

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Tuteketeze Mifumo

Afrika tunalaumiwa kuwa tunatumia muda mwingi kulaumu Wakoloni badala ya kutatua matatizo yanayolisibu Bara hili. Ni kweli wakati umefika wa kuwajibika kwa matatizo yetu. Lakini jambo moja tukumbuke, Ukoloni ndiyo uliopanda mbegu ya matatizo tunayoyaona katika Afrika. Ni kweli siyo tu tunawajibu wa kutatua matatizo yetu bali pia tunawajibu wa kufahamu ni wakati gani tulipoanza kunyeshewa mvua, ni kwa njia hiyo ndipo tutafahamu wakati wa kukauka.

Kama kuna ugomvi wa mipaka katika Afrika, kwanini tusiwanyoshee kidole Wakoloni, kwani kabla ya 1884(Mkutano wa Berlin uliogawa Afrika) hapakuwepo mipaka katika Afrika.

Mifumo waliyoacha wamejenga Wakoloni. Inaendelea kututafuna hadi leo. Chukua mfano Wagawe Uwatawale. Kwa makusudi walipandikiza, ukabila, uhasama wa Dini na maradhi hayo yanatutafuna na tumepoteza wazalendo wengi wa Afrika kutokana na sera hii waliyoacha wameiweka katika Afrika.

Ukisikia ukabila umeshamiri wala usijihangaishe ni hila waliyofanya. Kabila moja kulipa elimu na wengine kuwanyima na kabila moja kufundishwa kuwa wao ni bora kuliko jingine. Basi leo vyama vya Siasa, vyeo bado vinaendelea kutiririka katika mkondo huo wa ukabila na kusababisha maafa makubwa.

Hivi leo hatuna lugha yetu moja. Hawa wanazungumza kimombo, wengine kireno, acha wale wanaokimimina Kifaransa. Kweli mnara wa Babeli utajengeka bila lugha moja? Ukoloni huo wa lugha kauleta nani kama sio hao wanaotuona hivi leo hamnazo?

Matatizo na maumivu yanayoendelea nchini Sudan kwa hivi sasa unawezaje kuyaeleza vizuri bila kueleza Hisitoria ya Ukoloni? Nchi hiyo ya Sudan ambayo ni kubwa kuliko nchi nyingi katika Afrika, inayo historia ya kusisimua. Kwa Karne nyingi Sudan ilikuwa na falme Tajiri na maarufu kama Kush. Meroe, Napata, Funi, Dia Masahi, Darfur Falme hizi zilipata maendeleo makubwa katika nyanja za Kidiplomasia, biashara na utamaduni. Toka 1821 maafa yalianza ya utawala wa Ottoman uliendelea hadi 1898 uingereza ilipotawala nchi hiyo hadi 1956 Sudan ilipopata Uhuru wake. Toka 1898 hadi 1956 Mwingereza alipanda mbegu ya Ukabila, Utaifa, Dini alihimiza zaidi utawala wa kikabila na Koo. Wananchi wakawa na mapenzi zaidi na tawala zao za kikabila na Koo kuliko serikali kuu huko Khartoum. Kiini cha matatizo ya Sudan kinachimbuka kutokana na mfumo huo ambao madaraka yake Khartoum na wala uongozi huutilii maanani kilio cha watu. Malalamiko hayo yameendelea na kuvunja kabisa daraja la kuunganisha Khartoum na Majimbo na tawala za koo.

Kosa moja kubwa tulilolifanya katika Afrika ni kwamba hatukuvunja na kuteketeza mifumo tuliyorithi kutoka kwa Wakoloni. Mifumo inaendelea ile ile kilichobadilika ni rangi za watawala, lakini mateso na uonevu ni ule ule.

Wakati umefika kwa Afrika kubomoa mifumo iliyoachwa na Wakoloni kwani, ile ilitengenezwa kwa ajili ya manufaa yao na sio manufaa yetu. Bila kubomoa mifumo hiyo, maana yenyewe ya Uhuru itapotea kama bado haijapotea.

Wakati tunaendelea kuwatupia jiwe Wakoloni, tuone aibu kidogo. Inakuwaje Afrika ambayo watu wake wako taabani, ina viongozi ambao ni matajiri kuliko viongozi wengi Duniani? Kwanini waafrika wanashinda kutwa kucha kwenye ofisi za balozi za waliotutawala wakiomba Viza na wengine kutumbukia baharini kujipeleka utumwani kwa hao waliotutawala? Tunaendeleaje kuwa na hamu na vitu ambavyo hatuna uwezo navyo? Magari ya kifahari? Na mate kutudondoka kwa vile ambavyo hatuzalishi? Haya ni maswali yanayohitaji majibu.



QUR'AN TUKUFU

مَّن ذَا الَّذِي يُقْرِضُ اللَّهَ قَرْضًا حَسَنًا فَيُضَاعِفَهُ لَهُ وَلَهُ أَجْرٌ كَرِيمٌ)

Ni nani anayempa Allah karadha nzuri, ili Amzidishie. Naye pia ana ujira wenye heshina kubwa.

Al-Hadid (الحديد 11)



NUKUU YA HADITHI

عَنْ خُرَيْمِ بْنِ فَاتِكٍ، قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: مَنْ أَنْفَقَ نَفَقَةً فِي سَبِيلِ اللَّهِ، كُتِبَتْ لَهُ بِسَبْعِ مِائَةِ ضِعْفٍ
جامع ترمذی۔کتاب الجهاد۔باب فضل النفقة فی سبیل الله۔حدیث ۔1625.

Tafsiri: Imesimuliwa na hazrat Huraim bin Fatik r.a. kwamba Mtume s.a.w. alisema:" Anayetoa chochote katika njia ya Allah basi huandikiwa (malipo yake) mara mia saba.

Khalifatul Masih V^atba

Hazrat khalifatul Masih wa tano^atba alisema kwamba, hivyo basi kujitolea katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kwa ajili ya faida yetu.

Akikumbusha juu ya umuhimu wa kujitolea huku katika njia ya Mwenyezi Mungu, Masihi Aliyeahidiwa^as anasema;

"Haiwezekani kwenu muwe na mapenzi makubwa juu ya mali na wakati huo huo juu ya Mwenyezi Mungu. Ninyi mnaweza kupenda kitu kimoja tu."

Akasema tena; "Ni mwenye bahati kubwa yule anayempenda Mwenyezi Mungu, kama kati yenu kuna mtu anayejitolea mali yake kwa kumpenda Mwenyezi Mungu basi mimi ninaamini kuwa, bila shaka katika mali yake kutakuwa na baraka nyingi zaidi kuliko za wengine, kwa sababu mali haziji zenyewe bali zinakuja kwa matakwa ya Mwenyezi Mungu, basi mtu yule anayetoa sehemu ya mali yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu lazima ataipata, lakini kinyume chake mtu yule asiyefanya huduma kama ipasavyo, katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa sababu ya kupenda mali, yeye lazima ataikosa mali hii."

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Ukinaifu ndani ya Ndoa

Na.
Maulana Sheikh Shaban A. Shunda



Yatokapo hayawezi kurudi tena na athari yake haifutiki.
Hivyo ni vyema kabla ya kuongea maneno uyachuje kwanza akilini ndipo utamke na sio kuongea kila neno kwa sababu kuna mtu yupo mbele yako na ana masikio ya kusikia.
Inatakiwa wenzi muwe na siku au faragha za kuongea kiundani kuhusu mapenzi na hisia zenu za mmoja kwa mwingine, muda huo msahau kama mna majukumu wala shida bali muyaongee mapenzi na mahaba kwa undani wake, na siku hizo ziwe maalum na nyingi katika maisha yenu ya mahusiano. Mahusiano yenye mazungumzo kamwe hayawezi kuota kutu.

Kusomana Tabia
Ni jambo jema sana na muhimu kuzisoma tabia za mwenzi wako bila kujiingiza katika uchunguzi na ufukuaji ambao unaweza kuleta mtafaruku katika ndoa, ni vyema sana kujua apendacho na asichopenda mwenzi wako bila kumbugudhi na kujua ni jinsi gani ya kumtendea, mara nyingi wanaume hupenda tabia zao au maamuzi yao yaongoze Dola ya nyumba na wanawake hulazimika kwa kuogopa kuachika lakini namna hii itaenda mpaka lini? Uvumilivu una kikomo kwani hata bahari ina ukingo wake. Ni vizuri kusomana ili kujua kwani mtu anaweza kuambiwa tabia za mwenziwe akashangaa ila kama unamjua vyema unaweza kumrekebisha.
Kikubwa ni kupeana nafasi na kuweza kujenga jambo moja kwa pamoja ifike mahala ambapo mke na mume kuwa na tabia moja ambayo wameijenga kwa pamoja.

Kudhihirishiana Hisia
Ni muhimu sana kwa wanandoa kuendelea kudhihirishia hisia za upendo na kuonyesha kuhitajiana, kwani huenda ni nadra sana kwa wanandoa wanapozoeana kuambiana maneno matamu, au hata tu neno nakupenda na kuitana kwa majina ya kimahaba, kitu ambacho hupelekea yule nafsi mtoto ambaye yupo ndani ya kila mwanadamu kukosa chakula chake. Muda mwingine inahitajika mtu kuzivua fahamu zake na kujirudisha utotoni awapo na mwenziwe na kusahau na majukumu kabisa.

Kupeana zawadi
Zawadi ni njia nzuri ya kudhihirisha mapenzi yako na nafasi ya mwenzako katika maisha yako, na zawadi ambayo mtu huitoa kwa mwenzake bila ya utangulizi au mnasaba maalum huleta athari njema na huimarisha mapenzi. Na katika zoezi hili la kupeana zawadi, ni vema kila mmoja akaelewa anachokipenda mwengine ili zawadi iwe na athari inayotarajiwa, na iwe ni zawadi maalum kwa mlengwa, isiwe zawadi ambayo mtoaji naye atafaidika na zawadi hiyo, kwa mfano, si vema kwa mwanamme kumletea mkewe zawadi ya sufuria, microwave, pazia, Dinner set, hiyo haitaitwa zawadi, lakini ni juu yake kumletea manukato ayapendayo, hereni, bangili, mkufu au pete ya dhahabu, na vitu ambavyo ni maalumu kwa matumizi yake binafsi. Hali kadhalika kwa mwanamke kumzawadia mumewe achunge vigezo hivyo.

Kualikana vyakula
Inaweza kushangaza kuwa vipi wanandoa wataalikana chakula wakati wenyewe ni mume na mke, na ni lazima wale pamoja?! Ni vema ikaeleweka kuwa, kubadili mazingira na kufanya vitu makhsusi kwa kushtukizana, huwafanya wanandoa kutozoeana na kuchokana, kwani maisha yenye mtindo na mtiririko mmoja kila siku humfanya mtu kuyachoka, ni vema wanandoa na hasa mwanamke kuwa mbunifu katika kuyapaka rangi mpya maisha yao kwa kubuni vitu vitakavyo tia ladha mpya katika nyumba, njia mojawapo ni hiyo ya kumualika chakula maalumu mumewe peke yake, na hata kama itamlazimu kununua au kuagiza aina tofauti ya chakula basi afanye hivyo, na ampe mwaliko mumewe wa kutokosa kuhudhuria katika mnasaba huo. Aidha mwanamume naye anaweza kumualika mkewe katika hoteli ya heshima mlo wa mchana au usiku na kupata nafasi ya kujikumbusha mambo mazuri yaliopita.

Kubadilisha mpangilio wa nyumba
Wanawake wengi huwalalamikia waume zao kwa kutopenda kukaa nyumbani na badala yake kumaliza muda wao kwenye migahawa na kwa marafiki zao. Mke mwelevu huwa anafanya kila juhudi za kumnasa mumewe apende kukaa nyumbani wakati wa nafasi yake kwa kumbadilishia mazingira ya nyumba, kwani mazingira ya nyumba yanapokuwa ni yale yale tangu ndoa ilipofungwa hadi wanakuwa na watoto watatu, kochi lipo palepale kama kisiki cha mti, saa ya ukutani tangu imetundikwa mpaka imeshikana na ukuta, mapazia yaleyale na kama yanabadilishwa basi rangi ni zilezile, hali hii humfukuza mwanamume ndani ya nyumba na kumfanya arudi kuja kulala tu, na huu ndio mwanzo wa kuchokana na kuichoka nyumba.

Usafi wa mwili na mavazi
Moja miongoni mwa mambo yanayokera kwa wanandoa ni uchafu wa mmoja wao, uchafu ni sifa isiyovumilika hususan kwa mwanamke, baadhi ya wanawake hudhani kuwa manukato, vipodozi ndio usafi, utakuta anapitisha masiku bila kuoga kikamilifu, bali anapitisha pitisha maji na sabuni tu katika maeneo fulani, kisha kujijaza manukato, vipodozi na mafuta mengine, bila kuelewa kuwa, anapokuwa karibu zaidi na mumewe harufu ya asili hujitokeza na kuleta mchanganyiko wa harufu mbaya, hali kama hii si rahisi kwa mwanaume mstaarabu kuizungumzia kwa mkewe, atakaa nayo na atavumilia, lakini mwisho wake ni kumchoka mke huyu. Wanaume nao hudhani kuwa kwao wanaume ndio wamepewa kibali cha kuwa wachafu, kwa mfano wanaume wengi huona ni jambo la kawaida kunuka jasho, na wengine wana matatizo sugu ya kunuka miguu, huu ni uchafu ambao hauvumiliki kwa mwanamke msafi, aidha baadhi ya wanaume hawana vionjo katika mavazi yao, na jinsi wanavyojiweka, jambo ambalo linaweza kumsababishia mke maudhi, na hata kujihisi aibu kunasibishwa na mume wake.

Kufanya Ibada kwa pamoja
Nguzo muhimu na mhimili wa maisha ya ndoa ni kumcha Mungu/Allah, Sala za usiku humkurubisha mja karibu zaidi na Mungu, hivyo mume na mke kuhimizana kufanya ibada hii pamoja huwazidishia imani na mapenzi baina yao na kuifanya ndoa yao kuwa imara zaidi. Hii ndio njia ya mwisho na ya kwanza kama ikifanikiwa hamna tatizo.

Mwisho

Nidhamu ya Mpango wa Wasia

na Wajibu wa Musi

Kutoka Uk wa 1..

Utaratibu wa Wasia, huu ni kwa mali zote zinazohamishika na zisizo hamishika. Viwango hivi vya utaratibu wa utoaji wa michango hii ya wasiyyat ilielezwa na Masih Aliyeahidiwaás mwenyewe kwenye kitabu chake cha ***Al-wasiyyat*** sehemu alipotaja masharti ya kuzikwa katika makaburi ya ***Bahishti Maqbala*** (Sharti la pili, Uk;23). “Sharti la pili ni kwamba miongoni mwa Wanajumuiya yule tu atazikwa makaburini humu atakayefanya Wasia ya kwamba baada ya kifo chake sehemu ya kumi ya mali atakayoacha itatumiwa kwa kueneza Islam na kuhubiri maamrisho ya Kurani sawa na maagizo ya Jumuiya hii. Na kila mkweli mwenye imani kamilifu atakuwa na hiari ya kuandika katika Wasia wake zaidi yake vile vile, lakini siyo kidogo kuliko sehemu hiyo ya kumi.” ***(Al-Wasiyyat Uk: 23)***.

Utaratibu wa Kujiunga na Wasiyyat

1. Kusoma kitabu cha ***Al-Wasiyyat*** na kuyaelewa yaliyomo.
2. Kujaza fomu maalumu ya kukubali kuingia katika mpango huu wa kujitolea mali.
3. Lazima anaejiunga na Mpango huu wa Wasiyyat awe ni mtu anajibidiisha katika kuutafuta Ucha-Mungu

Masih Aliyeahidiwaás alielezea jambo hili kama ukumbusho kuwa

“Izingatiwe ya kuwa Haitoshi kutoa tu sehemu ya Kumi ya miliki inayoweza kusogezwa au isiyoweza kusogezwa, bali itamlazimu mwenye kufanya Wasia kadiri awezavyo, awe anatekeleza maamrisho yote ya lslam na kujibidiisha katika mambo ya Ucha-Mungu na utakaso. Awe Mwislamu, mwenye kumuamini Mungu kwamba yu Mmoja na amwamini Mtume wake barabara wala asiwe mwenye kunyang’anya haki za watu” **(Al-Wasiyyat Uk:31-32)**

Kujaza Fomu ya Wasia Kikamilifu.

- Muombaji aandike majina yake matatu sehemu ya kwanza ya jina.
- Tarehe ya kuzaliwa, tarehe ya Baiati, Kazi yake, Anuani yake vyote vijazwe kwa usahihi.
- Peni inayopendelewa kujaza fomu ni ya wino mweusi lakini ikikosekana basi itumike ya bluu pia.
- Peni ya wino mwekundu haitaikiwi
- Maandishi ya jazwe kwa herufi kubwa tu.
- Taarifa za mali zisizo hamishika ni lazima zijazwe; mfano Kiwanja, Shamba, Nyumba n.k sehemu ilipo, ukubwa wake na thamani yake kwa wakati huo.
- Dole gumba la mkono wa kushoto. Lazima Musi aweke saini yake na dole gumba kwa mwanaume na mkono wa kulia kwa mwanamke mashahidi wawili wa kiume ni lazima wapatikane waweke saini zao na dole gumba (wanapendelewa wawe ni watu wa Wasia).
- Saini ya Sadr wa Tanzimu ya muhusika ni lazima iwepo.
- Na maswali mengine yote ya fomu ni lazima yajazwe kwa uaminifu.
- Kama Musi ni Lajna na ameolewa, basi Mume ni lazima asaini na kutaja kipato chake

Muda gani Huchukua Kupata namba ya Wasiyyat

Kwanza ili kujua kuwa fomu uliojaza iko sahihi, baada ya kutuma fomu ya kujiunga na Wasiyyat Markaz. Markaz wanarudisha barua kwa muombaji kumueleza kuwa fomu yake imefika na inafanyiwa kazi au kama ina marekebisho basi marekebisho yafanyiwe kazi na fomu itumwe upya.

Barua hiyo ya majibu kutoka Markaz mara nyingi inaeleza kuwa, muombaji asubiri namba yake ya kukubaliwa Wasiyyat kwa muda wa kuanzia mwaka mmoja.

Ikitokea ndani ya kipindi hicho cha mwaka mmoja muombaji hajapata majibu ya namba ya Wasiyyat, basi taarifa zake zitumwe Markazi kupitia ofisi ya katibu wa Wasiyyat.

Hatua za kupata namba ya Wasiyyat huchukua muda mrefu hivyo kwa sababu ya taratibu za kisheria zinazochukuliwa na Markaz.

Wanaotakiwa Kujiunga na Mpango wa Wasiyyat.

1- Walipa michango.

Sawa na Maagizo ya Huzuratba anahitaii katika kila nchi, 50% ya walipa michango wajiunge na Mpango huu wa Wasiyyat.

2-Wafanya kazi wote wa Jamaat

3. Viongozi wa Majlis Amila zote, yaani Lajna, Ansarullah na Khuddam.

4. Watu wanaojibiidisha katika Ucha- Mungu

5. Wanaojiunga na Wasia waanzie umri wa miaka 15

Wasiotakiwa Kujiunga na Wasiyyat.

1- Mtu asiyekuwa Mwaminifu, Mwizi, Mdhulumati n.k

2-wasiolipa michango.

3-Mwenye Matatizo ya akili.

4. Mgonjwa mahututi asiyeweza kurudi afya yake ya awali.

Michango ya Wasiyyat.

Kwa ujumla kuna aina 3 za michango ya Wasiyyat

1. **Hissa Amad**- Mchango unaotolewa sawa na kipato. kwa kiwango cha Chanda Aam-mchango huu unalipwa endapo mali anayoimiliki Musi ina mpatia kipato kama Kodi, au mavuno n.k. Kiwango cha fedha kinachotakiwa kulipwa kwenye mchango huu ni 1/16.
2. **Hissa Jaidad**-Mchango unaotolewa sawa na mali isiyohamishika mara moja tu, katika kitu hicho.

HISSA AMAD

- Ni mchango unaolipwa kutoka kwenye kipato,
- Kiwango chake ni kuanzia 1/10 hadi 1/3. Report ya Hissa Amad uandaliwa na idara ya Wasia kila mwaka, ikiwa katika fomu ya Schedule C na CA kwa ajili ya kukaguliwa na Musi husika, kasha isainiwe na itumwe Markaz.
- Kwa watu wa mjini ni vizuri kipato kikalipwa kila mwezi na watu wa vijijini angalau kuanzia miezi 3, miezi 6.

Picha. Uk.08; Jedwari. H/A.01

HISSA JAIDAD

- Mchango huu hulipwa kutoka katika mali zisizo hamishika, mfano; Nyumba, Kiwanja na Shamba
- Ulipwa mara moja tu. Mchango huu una utaratibu wa ulipaji.

Taratibu za Kulipa Hissa Jaidad

1. Musi anatakiwa aandike barua kwenda kwa Amir Sahib ya kuomba kufanyiwa tathmini ya mali yake kwa ajili ya kuanza kulipa Hissa Jaidad.
2. Barua ya Tathmini ya kingereza itasainiwa na Musi ili kutuma ombi lake hilo Markaz.
3. Amir Sahib kupitia kamati ya Tathmini, itasimamia zoezi zima la kutathmini mali ya Musi na ripoti ya Jaidad anayotakiwa kulipa itatumwa Markaz.
4. Baada ya majibu kurudi, Musi atatakiwa kulipa Jaidad yake ndani ya Miaka miwili.
5. Kisha mara baada ya kumaliza ulipaji wa michango yake ya Hissa Jaidad, makao makuu watamtumia Musi cheti chake cha Hissa Jaidad

HISSA AMAD Katika Kiwango cha chanda Aam

• Ikitokea kuwa Musi anapata kipato, lakini pia ana pokea kodi kutoka kwenye mali yake fulani. Anatatiwa kulipa mchango wa kodi wa utaratibu wa 1/16

Kuuisha Taarifa za Mali Mpya.

• Kila baada ya miaka mitatu, Musi anatakiwa kuhuisha taarifa za mali yake Markaz. Au endapo Musi atapata kumiliki mali yoyote mpya isiyohamishika na inayohamishika wakati wowote anatakiwa kutoa taarifa ya mali hizo.

• Taarifa hizo zitajazwa katika fomu maalumu na kutumwa Markaz.

CHETI CHA WASIYYAT

• Mara baada ya hatua zote za ujazaji wa fomu ya kujiunga na Wasiyyat kukamilika, Makao makuu watamtumia Musi cheti chake cha Wasiyyat atakachokitumia kwenye changamoto yoyote ya Wasia wake.

• Madeni yote ya Musi yanatakiwa kulipwa ndani ya mwaka mmoja ili Wasiyyat wake uhesabike kuwa hai.

• Ikiwa Musi anataka kuzikwa katika Makaburi ya Bahishti Maqbara Qadian. Taratibu zote za gharama za kusafirisha mwili zitafanyika na ndugu zake mara baada ya kufanya mawasiliano kamili na Makao makuu na mwili wa marehemu utahifadhiwa kwenye Sanduku maalumu la kuzikia.

Sambamba na Hilo ikiwa Musi mwenye sifa atafariki sehemu nyingine mbali na Qadian na hakuzikwa kwenye Bahishti Maqbara ya Qadian. Ikiwa ametimiza sifa zote za Wasiyyat wake, hapo jiwe la kumbukumbu litawekwa katika makaburi ya Bahishti Maqbara Qadian.

Endelea Uk wa 9..

Ahmadiyya Mpigania Uhuru

Na.
Mahmood Hamsin Mubiru
Kiwalani Dar es Salaam

...Kutoka tolro lililopita

Wakajiunga na TANU ili kutetea heshima ya mtu mweusi

Mtemi Muhamed Kalubya alielewa kwa haraka falsafa ya



TANU kwani katika Islam Allah ni Rabbil-alamiina, ni muumbaji wa kila kitu Weupe, Weusi sote tumeumbwa na Mungu mmoja na ubora wa watu hautokani na rangi au kabila.

Uchamungu alikumbuka pia kuwa Mtukufu Mtume Muhammadsaw alijiunga na Chama cha kutetea wanyonge hivyo Mtemi Muhammad Kalubya alipojiunga na TANU alitumika kwa moyo wake wote, kwani alielewa kulikuwa na chombo chenye shabaha ya kurejesha heshima ya binadamu iliyoporwa.

Hakuna nguvu iliyoweza kuzuia wimbi hilo la hasira dhidi ya ukoloni. Kwa ustaarabu wa juu na lugha ya kiungwana TANU ulifafanua madai yake. Madai yalikuwa wazi na yalikuwa yamesababishwa na wao Wakoloni. Kukawa sababu ya kukubalika na kuheshimika kwa TANU kuliwapa tumbo joto wakoloni kama mfamaji ambaye hung'ag'ania kijiti akidhani ni mlingoti. Maofisa wengi wa Ukoloni walikuwa na chuki na wapigania Uhuru.

Walijiaminisha kuwa utawala wote na Wananchi wote isipokuwa wapigania Uhuru walikuwa wakorofi, inaonesha ya kuwa katika mapambano mkianza kubatizwa lakabu ya ukorofi, uchochezi, ugaidi uelewe mapambano yanakwenda vizuri na Weusi ukizidi basi elewa alfajiri iko karibu. Ni kanuni inaendelea hadi leo.

Kwa vyovyote Wadhalimu hufanya imafaima wabaki madarakani,hekima na busara vyote vinapita dirishani wanabaki weupe wa fikira. Wimbi hili la watu wanaoingia TANU makundi makundi tutalifanyaje lakini wengi wanaojiunga siwakina Yakhe. Sasa hii ikafanya wanyimwe taa wabaki gizani. Wafanya kazi wa Serikali, wakiwemo Waalimu waliamliwa kutokujiunga na chama chochote cha siasa, nia ilikuwa ni kutowapata wasomi katika uongozi wa TANU.

Wazalendo ilibidi waamue na wengi wakafanya uamuzi wa busara wa kujiuzulu na wengine wakaendelea kukiunga mkono kwa siri. Ni kana kwamba ulikuwa umemwaga Petroli kwenye nyumba inayowaka. Mkutano ulienda usiku wa manane wakipanga mikakati ya Ukombozi. Mwaka 1954 huo ilipozaliwa TANU wakaona wakimalize kingali kichanga. Mambo wakayafanya kuwa magumu. Ingawaje TANU kilisha sajiliwa rasmi, kila kilipo funguwa tawi ilibidi liandikishwe kabla halijaanza kazi, 1955 Sheria ya uchochezi ikapitishwa na 1955 ikapitishwa Sheria kuhusu kuchapisha kukusanyika ila wakasema raia wema hawana cha kuogopa desturi na kanuni ya wakandamizaji kuyapa uhalali matendo yao kwa kutengeneza Sheria ya kidhalimu. Tulianza tulipopata Uhuru na Sheria ya kumuweka ndani mtu kwa usalama wa Taifa. Mila na desturi za watawala wote ni kutumia Sheria kuhalalisha ubabe wao.

Lakini historia inatusaidia upande huo hufa kwa upanga, anayeishi kwa upanga katika hili historia haina ubaguzi inamtendea haki kila anayestahili.

Usishangae basi ukiona watu wanakimbilia kwenye Chama ambacho Sheria zote zina lenga wananchi wanaelewa kuwa hatimae kinacholengwa sio Chama bali wapenda uhuru na haki. Wimbi kama ulivyosema tufani Sheria hizi uonevu kamata kamata ya viongozi mbinu za kudhofisha Chama chao kwenye Donda imewekwa msumari wa Moto.

Hasira zikaongezeka Wananchi wakaimalika hali ikawa nzito na tete. Serikali katika sintofahamu aliyoingia Machela kurudi nyuma tabu Kwenda mbele mashaka. Serikali ikaona ni wakati wa kuwatumia watemi waliokuwa wanakubalika na kuheshimiwa. Katika mwaka 1957 ilipitishwa Teritorial Convention of Chiefs. Mara kwa mara Watemi walikutana na kujadili sera za Serikali kwa maelezo ya Wizara wataongoza mazungumzo ya kisiasa katika kiwango cha jimbo.

Hayo maoni ya kuchukuliwa Serikali nia ya Serikali iungwe mkono na Watemi ni viongozi wa kisiasa na kiroho utawala wa kikabila ndio jiwe la pembeni la Maisha ya Waafrika. Watemi ni sehemu muhimu ya mfumo huo ili watu wajue kuwa Serikali inawatambua na kuwaheshimu.

Serikali ilienda zaidi ya hapo. Ilitekeleza mpango wa kuwalipa. Mpango huu ulikuwa ni mbaya na mchafu na ulitaka kuendeleza ukoloni ukitumia vibaraka wa ndani. Huu ulikuwa ni mwendelezo wagawe utawala watie katika mgogoro wa ukabila watie katika mifuko kama senene na wawaache waumane baada yakuungana na kumshambulia aliyewaweka kwenye mfuko.

Baadhi ya watemi walielewa mtego huo na hawakukubali kuingia katika mtego huo. Miongoni waliokataa ni pamoja na Mtemi Abdallah Saidi Fundikira, Mtemi Harun Lugusha na Mohamed kalufya Mikutano hiyo ya watemi haikuwa na mvuto wakoloni ni heri kutengeneza nyama nyingi.- Wakiwa bado kwenye wazo lao la wachache kuwatawala wengi mwaka 1956 kulianzishwa Chama cha walowezi - United Tanganyika Party chini ya kivuli cha Gavana Sir Edward Twinning na kiongozi wa Chama hicho Iror Baylodon. Kimsingi kilikuwa Chama cha walowezi waasia na baadhi ya machifu walikaribishwa. TANU na UTP vilijiandaa kwa uchaguzi wa 1958.

Bado waliendeleza mbinu zao za kuweka masharti magumu. TANU ikaitisha mkutano Tabora ilikuwa patashika na baadhi ya watu walishauri uchaguzi ususiwe. Nyerere alijenga hoja waingie kwenye kura ya Mesto ni dhahiri nia haikuwa nzuri Mgombea uwe na pato la paundi 200 kwa mwaka, awe amemaliza darasa la 12, uwe umeajiliwa miongoni mwa mbilikimo unataka Mheshimiwa awe kama mtusi wa Rwanda. Si kioja hicho. Hata hivyo TANU ilishinda. Mara baada ya ushindi haikuchukuwa mda Tarehe 04/10/1958 Sir Richard Turn bull akatangaza kuwa Tanganyika itakuwa nchi ya walio wengi -Waafrika huo ulikuwa mgeuko mkubwa wa Sera ya Waingereza. Tanganyika katika kipindi cha miezi 38 likatoka tangazo hilo.

Tanganyika ilipata Serikali ya madaraka February 1959 na Uhuru kamili Tarehe 09/12/1961. Mkono wa watemi katika kurahisisha Uhuru wa Tanganyika ni mkubwa sana.

Walikataa kuburuzwa na wakoloni Uchaguzi wa 1958 kwa msaada mkubwa wa Watemi TANU ulijipambanua kuwa ni ya watu na inakubaliwa. Kwa uchaguzi huo Serikali ya kikoloni ilisalimu amri. Wakakubali yaishe. Wakafanya kila njia kujitafutia sifa ya kuuambia ulimwengu linalojili katika Demokrasia ya Magharibi. Hivyo walitakiwa kuendeleza urafiki huo wa kihistoria na wapigania Uhuru wangeendelea kuwategemea.

Nadhani juu ya Julius Nyerere walijuta. walikumbuka maneno ya Shakespeare katika Macbeth ***''There is no art to find the minds construction in the face. He was a man whom i had built absolute trust ''***

Hakuna mbinu ya kufahamu yaliyomo kichwani mwa mtu. Ni mtu tuliye muamini sana.

Bustani ya Washairi

Kwa Huku Haisikiki

Niwie radhi Mudiri, maandiko haya shika
Halafu uyahariri, fikisha kwa wahusika
Nao watupe khabari, Radio kutosikika
Radio Ahmadiya, kwa huku haisikiki.

Mtwara wafurahia, inasikika vizuri
Kadhalika na Songea, mambo ni kama sukari
Na Lindi wanachekea, vipindi wanakariri
Radio Ahmadiya, kwa huku haisikiki.

Kama ni kweli sijuwi, lakini kuna buruji
Inasikika Malawi, Angola na Msumbiji
Yasemwa imestawi, unasi yawafariji
Radio Ahmadiya, kwa huku haisikiki

Tunajua kuna vitu, vizito afanaleki!
Wanapelekewa watu, wale wapingao haki
Uhondo huo baratu, twapunguziwa ashiki
Radio Ahmadiya, kwa huku haisikiki

Haisikiki kabisa, sababu zake ni nini
Masafa yana makosa, au kuna kitu gani
Mitambo si ya kisasa? Kumbe tatizo ni nini?
Radio Ahmadiya, kwa huku haisikiki

Haisikiki Rufiji, Dar na Kaskazini
Morogoro na Ujiji, Bukoba na visiwani
Dodoma wanahitaji, waila Lo! Maskini
Radio Ahmadiya, kwa huku haisikiki

Polepole ndiyo mwendo, hajikwai mwenda pole
Ajikwaapo si ngondo, havunji vyake vidole
Nayafunguke mafundo, tukifikie kilele.
Radio Ahmadiya, kwa huku haisikiki

Al-Ustadh Mhenga
Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile – Mbagala Rangitatu.
Dar es Salaam.

Ni kanuni yake Mola

Sifa njema kwa mwenyezi, muumbaji na kupanga
Kanuni ndiye mjenzi, kwazo viumbe tufunga
Tunda huja kwa msimu, ni kanuni yake mola

Maembe yawe navua, machungwa yaje na jua
Ni kanuni ya jalia, viumbe tunatumia.
Tunda huja kwa msimu, ni kanuni yake mola.

Tunda huja kwa msimu, laimani au mwili
Maovu yanapotimu, laimani linajili
Tunda huja kwa msimu, ni kanuni yake mola

Kwaidhini ya manani, tunda laanza kumea
Njano yakuwa kijani, Amani inarejea
Tunda huja kwa msimu, ni kanuni yake mola

Zama za ujahilia, Imani lipopotea
Ndipo tunda kachipua, shiriki kuifukia
Tunda huja kwa msimu, ni kanuni yake mola

Msimu umerejea, kama wakale wa Musa
Yesu ameshatujia, zama hizi kutakasa
Tunda huja kwa msimu, ni kanuni yake mola

Msimu huu wa yesu, yule anayengojewa
Ahamadi ndiyo yesu, kaja alokingojewa
Tunda huja kwa msimu, ni kanuni yake mola

Mtunzi
Masihi omary stambuli kisagwa

Bishara imetimia

Siku muhimu ya leo, sawa na historia
Tarehe kama ya leo, bishara kainadia
Mola tampa mzao, dini taitumikia
Bishara imetimia, leo twasherehekea .

Seyyidina ahmadi, aliambiwa na mungu
Mwana aliye mweledi, atapewa jema fungu
Jamati atainadi, china hata kwa wazungu
Bishara imetimia, leo twasherehekea.

Ndani ya miaka tisa, mwenyezi alitamka
Kitakamilika kisa, mwana ataja oneka
Masihi aliwahasa, wahindu wenye haraka
Bishara imetimia, leo twasherehekea

Leo twasherehekea, bishara kukamilika
Yote yameshatimia, yalonenwa na rabuka
Elimu kaizamia, inashangaza hakika
Bishara imetimia, leo twasherehekea.

Jamati kaieneza, ulaya na afirika
Kila alililoliwaza, halikukosa Baraka
Mola aliye muweza, kamkuza kwa haraka
Bishara imetimia, leo twasherehekea.

Ni matukio lukuki, mola aloahidia
Kumaliza sidiriki, yote kuyahadithia
Bali naapa kwa haki, bishara imetimia
Bishara imetimia, leo twasherehekea.

Mwl.Mustafa Mambo Sahib
Sauti Nyembamba
Likokona Jamaat

Kumbe

Kumbe tungali Pamoja ,ijapo umeondoka
Kwa vitendo vyako mja,bado tuna kukumbuka
Shajarati kwetu tija ,Matunda twafaidika
Mti ulioupanda , thamarati twafaidi

Kifo hakitakuja, daima waheshimika
Si huzuni si Faraja, rohoni hujabanduka
Kwenye njozi unakuja, Kukumbusha kuishika
Kamba ile Madhubuti, Jinai lake Ukhalifa.

Mahmood Hamsini Mubiru (Wa Mamba)
Mgombani, Kiwalani.

Naomba Munieleze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Kila Kitu kiwesawa, maumbile tusawaze?
Majukumu yawesawa, Wana tuwanyonyesheze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze?
Kulima tufanye sawa, kupika nakozamuze
Sauti zipande sawa, siwepo naapunguze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Auviti viwesawa, vyeo tukigombeaze
Wasosifa kiusawa, mamlaka tuwajaze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Baba mama wawe sawa, sauti tuzipuuze
Nayemama awesawa, ubini tumuitize

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Au ndoa ziwesawa, mke namke tuoze
Wanaume naosawa, mume kwa mumetuoze

Haki sawa ndio Nini, naomba munieleze
Mabingwa wahaki sawa, kinyume munieleze
Hukunaku kuwe sawa, mlingano idadize.

Mtunzi
M.O.kisagwa

Ndoa za Utotoni

Nakupenda Tanzania, tunapendana
Naandika ninalia, ni msichana
Ni mengi yanatokea, kuozeshana
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Bibi ananisumbua, kwa kunifata
Shule nikijirudia, mbona najuta?
Sadiki akungojea, utamkuta
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Mama nae majanga, anapayuka
Kidawa uvae shanga, umeumbika
Mwenzenu nina majanga, patasomeka?
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Kusoma sio lazima, wameng'ang'ana
Juma mtu mwenye wema, hatakukana
Wataka chochote sema, atapambana
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Wacha nisome jamani, ni haki yangu
Mnanijaza kichwani, manyungu nyungu
Unyago wa kazi gani, kiulimwengu?
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Kunikeketa hapana, mwanionea
Mnaua usichana, najililia
Namuomba Subuhana, nawasemea
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Mnanijaza kichwani, vyenye ujinga
Shangazi unatamani, ndoa kufunga
Bado niko masomoni, sijajifunga
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Mamdogo Rebeka, ananifata
Olewa uje kudeka, ananisuta
Ananiingiza chaka, mbona najuta?
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Dada yangu Rashina, ananikosha
Ananipa nguvu sana, anibebisha
Asema nisome sana, anaikumbusha
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Nyumbani hapakaliki, kunisemanga
Wajomba hawashikiki, wanibolonga
Olewa uache dhiki, wananizonga
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Jirani zetu wanoko, wanachagiza
Wamemisi mualiko, waje kucheza
Wana haraka kuliko, 'mepitiliza
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Tunu ameshaolewa, kalazimishwa
Wanamwambia ngekewa, naogopeshwa
Sitetewi na wandewa, ninayumbishwa
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Serikali yangu pendwa, nihurumie
Hata kusoma nashindwa, unitetee
Hizi ndoa umeshindwa?, uniambie
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Twanyanyasika wadada, kwenye majumba
Wanasema tutadoda, tuwe wachumba
Niolewe wanywe soda, nibebe mimba
Ndoto yangu inazimwa, kunilazimisha ndoa

Nawasihi waungwana, tulizaneni
Mimi bado msichana, niko ndotoni
Ninaota kwa mapana, niwe chuoni
Ndoto yangu inazimwa, kisa nipatiwe bwana

Abdallah Kalindima
#CHUMACHAKAVU
Kalindimasenior@gmail.com

Mbwa Mwitu Na Kunguru

Palikuwepo na kunguru akiwa amekaa kwenye tawi la mti na kipande cha mkate mtamu uliopakwa samli mdomoni mwake. Mbwa mwitu alimuona kunguru na ule mkate na akaanza kutafakari namna ya kufanya ili aupate ule mkate.

Akasogea karibu na kusimama chini ya mti akitazama juu na akasema, "Ndege msharifu namna gani nimuonaye juu



yangu! Uzuri wake hakuna wa kufanana naye, rangi ya manyoya yake ni tamu sana. Laiti kama utamu wa sauti yake unalingana na uzuri wake, basi bila ya shaka yoyote anapaswa kuwa malkia wa ndege". Kunguru alifurahishwa mno na sifa hizi, na ili tu kumuonyesha mbwa mwitu ya kuwa anaweza kuimba alitoa mlio mkubwa sana. Kipande cha mkate kikamdondoka hadi chini, mbwa mwitu akikiokota kwa madaha sana alisema, "Una sauti dada, naona. Unachohitaji sasa ni akili tu."

. . . . . .

Hadithi hii inatufundisha nini?

Maadhimisho ya Ukhalifa

yafana Mkoani Ruvuma

Kutoka Uk wa 01..

mwenyewe, lakini kuna tofauti katika missing yake. Utume unakuja wakati ule dunia imejaa ufisadi na uasi, Shirki na giza la imani lipo kila mahali. Hivyo kwa wakati kama huo, uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu hudhihirika katika mfumo wa kuleta utume duniani. Pia kwa upande mwingine, uwezo wa Allah Taala hudhihirika kwa namna ya ukhalifa kwa maana ya kudra ya pili ambapo Jamaati iliyoanzishwa na Mtume ambayo inatimiza masharti ya imani na matendo mazuri lina pata kiongozi toka miongoni mwao ili kutimiza bishara na matakwa ya mwenyezimungu ambayo hayakutimia wakati wa uhai wa Mtume.

Na hii ndiyo sababu ya kuwepo tofauti katika njia ya kumchagua Mtume na Khalifa. Mtume anachaguliwa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu, kwa sababu katika kipindi hiki cha giza, mkusanyiko wa waumini haupatikani, na baada ya kuja kwa Mtume, umati wa waumini unaundwa, na baada ya kifo cha Mtume, Mwenyezi Mungu kwa upendeleo wake, anaweka mfumo wa ukhalifa katika mkusanyiko huu wa waumini. Na umma huo wa waaminio unatimiza masharti ya imani na matendo mazuri kwa njia inayomridhisha Mwenyezi Mungu.

Hakika swali hili lipo wazi kabisa kwa kila mwislamu **kwamba Makhalifa walipatikana katika Islam** na kwa idadi yao walikuwa wanne tu baada ya kifo cha mtume saw lakini kuna bishara ya kupatikana tena katika zama za mwisho.

Nita wataja hapa pamoja na zama walizo dumu katika uongozi au kiti cha ukhalifa

1 **Hadhrat Abubaka Swiddiq r.a aliongoza katika kiti cha ukhalifa toka tarehe 8 June mwaka 632 hadi tarehe 23 mwezi wa tisa mwaka 634. Yeye alizaliwa tarehe 27 / 10 / 573 na akafariki tarehe 23 mwezi wa tisa mwaka 634 akiwa na umri wa miaka 60.**

2 **Hadhrat Omar Bin Khattab r.a aliongoza toka tarehe 23 mwezi wa tisa mwaka 634 hadi tarehe 3 / 11/ 644. Yeye alizaliwa mwaka 582 au 583 sawa na tofauti za kihistoria na alifariki mwaka 644 tarehe 3 mwezi wa 11 katika mwezi wa dhul hijja akiwa na umri wa miaka 61.**

3 **Hadhrat Othman Bin Affan ra alianza kuongoza tarehe 6 novermber mwaka 644 hadi tarehe 17 June mwaka 656. Alizaliwa mwaka 576 kabla ya hijiria na kufariki 17 June mwaka 656 katika mwezi wa dhul hijja akiwa na umri wa miaka 83.**

4 **Hadhrat Ali Bin Abii Twalib r.a aliongoza toka mwaka 656 hadi tarehe 28 mwezi January mwaka 661 akiwa na umri wa miaka 60.**

3 Je katika zama za mwisho zipo ahadi zozote za uwepo wa khalifa.

Naam katika zama za mwisho upo utabiri ambao Mtume Muhammad saw alibashiri uwepo wa ukhalifa chini ya kivuli cha unabii. Jambo hili lina kubaliwa na wanazuoni wote wa kiislsm na waislam kwa ujumla kuwa kuna zama zitakuja na maranyingi wamehangaika kuuhuisha ukhalifa huo bila mafanikio kwa sababu wale wanao taka kuusimamisha ukhalifa wanakiondoa cheo cha unabii na kutaka ukhalifa ujitegemee na ni jambolisilo wezekena kwa mujibu wa kanuni za kibishara na dini kwa ujumla. Kwanza tuangalie ndani ya Quran Mwenyezimungu anatwambia nini **katika sura nnur 24 aya ya 56 kuwa Na Allah amewaahidi wale walioamini na kufanya vitendo vizuri katika ardhi Bilashska atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyo wafanya wale wa kablayenu, Na kwayakini Ata waimarishia dini yao Aliyo wapendelea na Atawabadilishia Amani baada ya hofu yao. Na atakaye kufuru Baada ya hayo , basi hao ndiyo wavunjao Amri [sura nnur 24 aya ya 56]**

❖ **Hapa kuna point kadhaa tuzieleze kwanza**

1 Sharti lakwanza watu wawe waaminio yaani walio mwamini Allah na mtume wake kisha wakafanya vitendo vizuri. Kwahakika ni sharti walilopewa waislam ili wapate neema hiyo ya ukhalifa, na kwahakika shirti hili lina walenga waislam moja kwa moja kwa sababu Allah ana wafananisha na

Itaendelea..... toleo lijalo Inshallah

Jifunze Kuchoma Mishikaki ya Kuku

Na **Mtandao**



Mahitaji:-

» Vidari vya kuku 2, bila ngozi wala mifupa (safisha na katakata vipande vidogo dogo)
» Mafuta 1/4 kikombe
» Chumvi na pilipili manga kiasi
» Kitunguu saumu kilichopondwa kijiko 1 1/2 cha chai
» Tangawizi ilosagwa 1/2 kijiko cha chai
» Maji ya limao 1 dogo au 1/2 kubwa
» Majani ya kotmiri yalokatwa katwa kiasi

Namna ya Kutayarisha:

1. Tia kuku wako pamoja na viungo vyote katika bakuli na changanya vizuri kwa mikono viungo vienee.

2. Funika vizuri na wacha viingie viungo kwa muda wa saa moja unaweza pia kuacha usiku kucha katika fridge kwa ladha zaidi

3. Ukitumia vijiti vya mti basi hakikisha unaviloweka katika maji baridi kwa muda wa nusu saa ili visiungue wakati wa kuchoma

4. Tunga mishikaki yako kwa idadi upendayo na kisha choma au oka hadi ipate kuiva vizuri pande zote mbili.

5. Mishikaki tayari kwa kula kwa sauce upendayo, ukitaka viungo zaidi unaweza tia manjano, binzari nyembamba ya unga na giligilani ya unga au uoendavyo. Furahia!

(kwa oveni moto uwe nyuzi joto 200)

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA^{AS}

KUISHI MAISHA YA UNYENYEKEVU NA UMASKINI

Kwa wacha Mungu kulikuwa na sharti hili kwamba waishi Maisha ya Unyenyekevu na Umaskini. Hili ni tawi moja la ucha Mungu ambalo kwalo tunapaswa kukabiliana na hasira isiyojuzu. Kituo cha mwisho na kigumu cha arifu na masiddiki ni kuepukana tu na ghadhabu. Kiburi na majivuno huzalika kutokana na hasira; na vivyo hivyo, wakati mwingine, hasira yenyewe inakuwa matokeo ya Kiburi na majivuno, kwa sababu hasira hutokea wakati Mtu anapojipendelea nafsi yake kuliko mwingine. (Taarifa ya Jalsa Salana, ١٨٩٧, uk. ٤٩)

Kama nyinyi mnataka Mungu Awe radhi mbinguni, basi mnapaswa muwe na umoja kama ndugu wawili wa tumbo moja. Aliyetukuza zaidi miongoni mwenu ni yule anayeyasamehe zaidi makosa ya nduguye, na mwenye bahati mbaya ni yule anayefanya ukaidi na hasamehi, basi huyo hahusiani nami. (Kashtie Nuh (Safina ya Nuhu), Ruhani Khazain, J. ١٩, uk. ١٢ -١٣)

Taasisi Ya Majlis Shura – Mashauriano

Kutoka Uk wa 11..

Umuhimu wa Kutekeleza Maamuzi ya Shura:

Hadhrat Khalifatul Masih^{atba} alisema kwamba wakati mwingine, maamuzi hayatekelezwi kikamilifu kwa sababu ya ulegevu na uzembe wa viongozi. Katika hali kama hizi, wajumbe wa Shura waelekeze wanachama wa jumla katika kutekeleza uamuzi huo, lakini wanapaswa pia kuwakumbusha wenye nyadhifa. Ikiwa licha ya hili uamuzi hautekelezwi, basi mjumbe wa Shura anapaswa kuandika kwa makao makuu. Kumbuka kwamba mtu anaweza kutoa visingizio vya kukwepa majukumu yake na kuyapuuza katika maisha haya tu, lakini wataulizwa na Mwenyezi Mungu juu ya majukumu waliyokabidhiwa. Hili ni jambo linalotakiwa kuangalia sana. Ikumbukwe pia kwamba mjumbe hatakiwi kuwasilisha malalamiko dhidi ya mwenye wadhifa fulani baada ya kutokea hitilafu ya aina fulani ya kibinafsi baina yao. Ni lazima daima wakanyage njia ya ucha-Mungu. Maamuzi yatekelezwe kwa kiwango hiki kwamba pendekezo hili lisihitaji kamwe kuwasilishwa kwa Khalifa wa Wakati tena, wala pendekezo hilo halipaswi kutumwa kwa maelezo kwamba kwa vile suala hilo lilikwishawasilishwa hapo awali, inapendekezwa kwamba lisiwasilishwe tena. Hudhur (atba) alisema kwamba hii inapaswa kuwa chanzo cha aibu. Lengo linapaswa kuwa kwa kitu kama hiki kamwe kusitokee.

Hudhur (atba) alisema kwamba inapaswa pia kuchambuliwa kwamba kunaweza kuwa na Jumuiya fulani hai zinazotekeleza kikamilifu uamuzi uliotolewa na Khalifa wa Wakati. Inapaswa kuonekana ni kitu gani kilichovutia kutekeleza maamuzi yaliyofanywa kwa moyo mkunjufu na kwa shauku na kanuni hizo hizo zishirikishwe na Jumuiya ambazo hazifanyi kazi vile ilivyo.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba hatuwezi kuleta mabadiliko katika ulimwengu kwa maneno tu, bali lazima tuonyeshe matendo yetu. Ikiwa wajumbe wa Shura watazingatia kuboresha viwango vya ibada zao na kuhudhuria msikiti, basi mahudhurio ya jumla yanaweza kuongezeka katika misikiti mara tatu. Ikiwa wajumbe wa Shura watawatendea wengine kwa huruma na upole na kuwaombea dua, na kama wataongeza kiwango cha utiifu wao kwa Khalifa wa Wakati, basi mabadiliko ya kimapinduzi ndani ya Jumuiya yanaweza kutokea. Tumekabidhiwa jukumu kubwa. Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alitumwa na ujumbe wa kueneza mafundisho mazuri ya Uislamu kwa ulimwengu na kuuleta chini ya Umoja wa Mungu. Utimilifu wa misheni hii unahitaji juhudi za mara kwa mara. Kutimiza malengo haya pia kunahitaji fedha. Kwa hivyo, wakati wa kujadili bajeti, ni lazima ionekane ni jinsi gani kazi nyingi zinaweza kufanywa huku wakiwa waangalifu katika matumizi.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) aliomba kwamba tuweze kutimiza wajibu wetu tunapokanyaga njia za ucha-Mungu. Mwenyezi Mungu Atufunikie mapungufu yetu na Aendelee kutumiminia baraka zake.

Muhtasari uliotayarishwa na
Mwisho

TANGAZO LA IJTIMAA YA MAJLIS KHUDDAMUL AHMADIYYA TANZANIA

Tanzim ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania inapenda kuwataarifu Khuddam na Atafal wote nchini kuwa Ijtimaa yao itakuwa tarehe 23 - 25 Juni 2023, Kitonga, Wilaya ya Ilala, Da. es Salaam.

In-Shaa-Allah.

Khuddam na Atfal wote wanaombwa kuendelea na maandalizi ya Ijtimaa hii na kuichangia pia sawa na matakwa ya katiba.

Usipange kukosa!

Limetolewa na Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania

FOMU ZA HISSA AMAD NA JAIDAD

Kutoka uk. 04

بسم الله الرحمن الرحيم

Ofisi ya Wasia

Jina: Wasia no. Jamaat:

S Na.	Swali	Jibu	Maelezo
1.	Bajeti yako ya mwaka 20__ July –20__ June ilikuwa kiasi gani? (Taarifa itoke katika fomu ya bajeti ya tawi. kwa hiyo wasliana na K/Fedha wa tawi.)		
2.	Sawa na taarifa zetu umelipa kiasi cha shillingi		
3.	Je ni Kweli au Hapana?		
4.	Kama, Hapana ni kiasi gani umelipa kwa mwaka 20__ July –20__ June.		
5.	Ambatanisha uthibitisho, aidha kopi ya risiti ya malipo ya kipindi hiki, au andika tarehe na namba ya risiti.		
6.	Sawa na taarifa kutoka Makao Makuu Rabwaha, deni lako kwa mwaka _____ July – _____June.		
7.	Sawa na taarifa kutoka Makao Makuu Rabwaha, ziada yako kwa mwaka _____ July – _____June.		
8.	Kama umelipa chini ya bajeti yako, tafadhili toa maelezo kwa nini imekuwa hivyo?		
9.	Kama umelipa kuzidi bajeti yako, tafadhali toa maelezo. Kiasi kilicho zidi ni malipo ya deni? Kiasi kilicho zidi ni malipo ya Hisa Jaidad? Au eleza chanzo cha malipo hayo?		
10	When was his data sent to markaz last time?		

- Tafadhali saini fomu Schedule C iliyoambatanihswa chini kulia kwenye mahali ilipowekwa alama ya ★ pia majina yako kamili pamoja na anuani yako kamili na tarehe.
- Kama kuna maelezo Zaidi kuhusu taarifa zako, tumia karatasi ya ziada na uambatanishe pamoja na fomu hii.
- ***Wanachama wa wasia wanapaswa kutunza shahada, barua na risiti zote za wasia wao kwani zinaweza kuhitajika wakati wowote kwa matumizi ya kiofisi.***

1.TAJA NAMBA YAKO YA SIMU_____

2.TAJA KAZI YAKO_____

kwa mawasiliano zaidi piga simu NO 0654081914 au 0623084840

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT - TANZANIA

SCHEDULE C (a) 2021-2022

RATE OF WASIYYAT

NAME: [redacted] WASIYYAT No. 114810

DATE			DATE	R/NO	AMOUNT
31st July, 2021	MD 7696	22,000	0	0	-
22.7.2021	129889	5,000	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
1/0/1900	0	-	31st January, 2022	MD 8608	22,000
0	0	-	17.1.2022	174592	12,000
0	0	-	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
0	0	-	28th February, 2022	MD 8765	22,000
0	0	-	20.2.2022	208106	2,500
31st August, 2021	MD 7847	22,000	1/0/1900	0	-
1/0/1900	174512	5,000	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
1/0/1900	0	-	31st March, 2022	MD 8922	22,000
1/0/1900	0	-	1/0/1900	0	-
0	0	-	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	1/0/1900	0	-
0	0	-	0	0	-
30th September, 2021	MD 7997	22,000	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
0	0	-	0	0	-
0	0	-	30th April, 2022	MD 9080	22,000
0	0	-	18.4.2022	208126	12,000
0	0	-	1/0/1900	0	-
0	0	-	1/0/1900	0	-
31st October, 2021	MD 8148	22,000	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
0	0	-	0	0	-
0	0	-	0	0	-
30th November, 2021	MD 8300	22,000	30th April, 2022	MD 9239	22,000
1/0/1900	174562	2,500	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
0	0	-	0	0	-
0	0	-	30th June, 2022	MD 9398	22,000
0	0	-	25.6.2022	208159	4,200
31st December, 2021	MD 8452	22,000	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	1/0/1900	0	-
1/0/1900	0	-	0	0	-
0	0	-	0	0	-
0	0	-	0	0	-
0	0	-	0	0	-
GRAND TOTAL					307,200

WAJIBU WA MUSI KWENYE WASIYYAT WAKE

• Kulipa michango yake ya Hissa Amad na Hissa Jaidad kikamilifu.
• Musi anawajibu wa kulipa mchango wake wa Hissa Jaidad angali yupo hai.
• Musi anawajibu kila baada ya miaka 5 kuitaarifu Idara ya Wasia juu ya mali mpya zilizoongezeka katika miliki zake.
• Kutunza kumbukumbu zote zinazohusu Wasiyyat wake. Kuanzia risriti za michango kila mwaka, taarifa za hesabu kutoka Markaz, Cheti cha Wasiyyat, barua ya kukubaliwa Wasiyyat, Cheti cha malipo ya kukamilisha Hissa Jaidad.
• Kuhakiki na kusaini taarifa za michango yake ya Hissa Amad inayoandaliwa na Idara ya Wasiyyat kila mwaka. Musi anawajibu wa kujua, Je hakuna ripoti yoyote ya michango yake ya Wasiyyat ambayo haijatumwa Markaz kwa miaka ya nyuma.
• Musi ana wajibu wa kuipa taarifa idara ya Wasiyyat endapo katika kipato chake kuna mabadiliko aidha ya kuongezeka kwa kipato au kupungua kwa kipato.
• Musi anawajibika kukagua wakati wote ulipaji wa madeni yake katika mchango wa Hissa Amad. Pamoja na kuhakikisha kuwa anayalipa kwa wakati.

CHANGAMOTO ZA IDARA YA WASIYYAT.

1-Fomu za hisabu hazisainiwi na Musi husika, mfano baadhi ya wakati ni walimu wa Jamaat usaini badala ya Musi.
2-Musi wengi hawajui viwango vyao sahihi vya ulipaji Hissa Amad.
3-Kiwango cha chini cha nchi yetu kwa ulipaji wa Hissa Amad ni 60,000/= kwa mwaka. Hivyo kama Musi atashindwa kulipa kiwango hiki atakuwa na deni la kulipa.
4-Musi awaelewi fomu za hisabu C na CA
5-Malipo ya Wasia deni au H/jaidad kutajazwa kwa ufasaha katika vitabu vya risiti.
6. Fomu nyingi na majibu yanayotoka Markaz hazifiki kwa wahusika kwa wakati.
7- Idadi ya Musi wengi kuto kuwa na namba za Wasiyyat, na baadhi ni kwa muda mrefu.
8-kukosekana na cheti cha Wasiyyat
9-Taratibu za H/jaidad kutofatwa
10. Fomu za Hisabu za Hissa Amad hazirudi kwa walkati
11-kukosekana kwa taarifa za vifo vya Musi mapema.

بسم الله الرحمن الرحيم

Details of Payments & Declaration Regarding Hisa Amad
Under Rule No.69 (Schedule C and C (a))
OFFICE OF WAKILUIL MAL THANI (II)

TAHRIK E JADID ANJUMAN AHMADIYYA PAKISTAN, RABWAH
DISTRICT CHINIOT, PAKISTANI

NAME..... WASIYYAT NO. .....

S/D..... FISCAL YEAR.....

ADDRESS..... RATE OF WASIYYAT.....

Declaration of the Musi/Musiah.

Source of income [ ] **Budget declared** [ ]

Please tick ☑ in the relevant box and also write the exact amount in filling space.

Keeping in view the above mentioned payments and comparing them with my total income during this year being regardful of the requirement of taqwa.

[ ] I have fully paid my dues chanda based on the total income delivered from various sources and there is no arrear or excess left behind.

[ ] The above shown payments include an extra sum of (currency)..... which is the payment of my past dues OR which I have paid intentionally. (*Please cut the irrelevant portion*)

[ ] I owed the arrears of (currency)..... Which I have now paid under receipt no. ..... Dated..... OR I will pay them within the next..... Months. (*Please cut the irrelevant portion*)

Signature of Musi/Musiah

★.....

Date.....

Signature of Amir Jamaat

Wasiyyat No						

WAKIL UL MAL(II)
TAHRIK-I-JADID
RABWAH-P.C.35460
PAKISTAN

PARTICULARS OF ESTATE & PROPERTIES

(Under Rule No.53)

Dear Brother, Assalamo Aleikum wa Rahmatullahe wa Barakatohu.

Please be informed that following are the particulars of my property at present. Kind, type, condition, area, situation etc, and approximate present value of each has also been stated:-

Residential plot/ Field/ House and Shop etc.	Agricultural land, Field etc.	Cattle	Shares/Bonds, Cash, Bank Deposit etc.	Investment in any other form	Jewellery, Ornaments

I have included all the Estate and Properties according to the Instructions (as given on the backside)

Name of Musi _____

Present Address: _____

_____

Permanent Address: _____

_____

_____

(Signature of Musi)

Date: _____

Kalamu kutoka Kanda ya Ziwa

...Kutoka tolro lililopita

KUCHANUA KWA CHEMCHEM YA JAMAAT AHMADIYYA MKOANI SHINYANGA - 4



Yousuph Mgeleka (Muijukuu)

Kwa kuona hali ya mahubiri mkoani Shinyanga inazidi kushamiri siku hadi siku, mpendwa kiongozi wetu wa Jumuiya nchini maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akona ipo haja sasa kuanzisha mkutano maalum wa kuwaleta pamoja wanajumuiya wapya wa mkoa wa Shinyanga yaani (Jalsa Nau Mubaein). Sisi kama wenyeji tukapokea na kutii maono ya mpendwa Amir sahib wetu, na kufanya mashauriano kwa kuanzia mkoani Mwanza ambapo ndio walikuwa walezi wa kijamaat kwa Mkoa wa Shinyanga. Kwa pamoja ikaridhiwa na kukubaliwa tufanye Jalsa Nau Mubaein, na eneo likatengwa. Ambapo ikashauriwa mkutano huo wa siku moja ufanyike katika kijiji cha Tinde mkoani Shinyanga sehemu ambayo ni katikati kufikika kiurahisi. Naam na ikawa hivyo.

Ifahamike kuwa lengo la mkutano huo wa kwanza ni kuwaleta wanajumuiya wapya mbele ya Amir sahib, kwa malezi. Alhamdulillah mkutano huo ukaandaliwa kwa mara ya kwanza katika ukanda huu wote wa Ziwa, na mkutano huo kufanyika katika kijiji cha Tinde mkoani Shinyanga. Maandalizi yalifanyika kwa kutafuta eneo la shule na kuomba vibali serikalini, na mara baada ya maandalizi kukamilika taarifa za mwisho zikapelekwa ofisini kwa Amir sahib na kuthibitisha uwepo wa mkutano huo ujulikanao kama Jalsa Nau Mubaein. Sisi wenyeji, tukaandaa kamati zetu (licha ya uduni wa uzoefu) katika kuendesha aina ya mikutano inayojumuisha umati mkubwa.

Tunashukuru mkutano huu wa kwanza kabisa ukanda wa Ziwa ulipata Baraka za uwepo wa kiongozi wetu mpendwa Amir sahib maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib ambae ni Amir na Mbashiri Mkuu mpaka sasa, huku akitoa ruksa kwa Maulana Sheikh Abdulrahman Ame sahib na Mwl Abdullah Mbanga sahib nao kuja kushiriki kwa mara ya kwanza mkutano huu. Mkutano huu pia ulipata Baraka ya kuhudhuriwa na Sadr Majlis Khuddamul Ahmadiyya (wakati huo) ndugu Twaaha Nyange sahib aliyeambatana na wajumbe wake akiwemo ndugu Abdallah Msesemele sahib, Jaafar Sandi sahib na ndugu Munawwar Mkoka sahib. Mkutano huo wa kwanza ulipata pia Baraka za kuhudhuriwa na Maulana Sheikh Waseem Ahmad Khan ambae ndio alikuwa amehamishiwa Mwanza akitokea mkoa wa Tabora, huku akiwa na jukumu la kusimamia mkoa wa Shinyanga.

Nakumbuka mkutano huo ulifanyika siku ya Jumapili, ambapo ndugu wengi walishiriki kutokea jijini Mwanza ambao walikodi bus ndogo aina ya Coaster ili kuja kushiriki na ndugu zao wanajumuiya wapya wa mkoa wa Shinyanga. Huku wanajumuiya wa Shinyanga kupitia matawi rasmi ya Negezi, Bugimbagu, Nsalala, Sungamile, Kidanda, Buchama wote walishiriki pasipo kuwasahau wenyeji wa kijiji cha Tinde yenyewe. Ikumbukwe wakati huo alikuwepo mwalimu akisimamia Mkoa wa Shinyanga ambae alikuwa ni Mwl Shaaban S. Lusseza sahib.

Wahudhuriaji wakawa ni kutoka rika zote lakini Lajna ndio walikuwa ni wengi zaidi, hivyo ndugu wote wakafika eneo la tukio. Kwa kuwa huu ulikuwa ni mkutano wa kwanza kabisa mbele ya Amir sahib, kulikuwa na udhaifu kidogo wa uzingatiaji wa muda ambapo ikalazimu mkutano kuanza majira ya saa nne badala ya saa tatu asubuhi. Na mkutano ulianza kwa washiriki wachache, lakini kufikia majira ya adhuhuri basi Alhamdulillah ndugu wengi wakawa wamefika na kushiriki. Mkutano huu ulikuwa ni wa siku moja tu.

Moja ya muujiza wa ukanda huu naokumbuka ni kwamba, mpaka kabla ya mkutano kuanza, hali ya hewa kwa mkoa wa Shinyanga ilikuwa ni kavu sana na mvua hazinyeshi. Basi tukafanya mkutano wetu katika viwanja vya shule huku vumbi likiupuliza mkutano tangu mwanzo, huku sisi pembeni tukijisemea mgeni wetu rasmi Amir sahib tumemualika kwenye vumbi hili lote. Lakini kwa kuwa ulikuwa ni mkutano wa kimbingu tukasema Allah ataubariki mkutano na atatubariki sote, kila kitu twamuachia Allah sawa na hali zetu. basi mkutano ule ukaendelea baada ya ufunguzi wake, na khotuba mbalimbali zikatolewa kwa muda wote mpaka mwisho. Mkutano ukaisha majira ya alasiri kwa kufanya maombi na kisha kusali swalat zote dhuhr na al asr kwa pamoja. Baada ya ibada ikafuata wasaa wa chakula, ambapo mgeni rasmi Amir sahib na ugeni wake wakapata chakula, lakini pia washiriki wote wa mkutano nao wakapata chakula.

Ile tu mkutano umeisha na ndugu wote kupata chakula, basi mvua kubwa sana ilinyesha kwa mara ya kwanza na kuleta neema. Neema ambayo ikageuka na kusemekana hawa waislamu leo wakuja kufanya mkutano hapa Tinde na mvua imenyesha, yaani wamemaliza tu mkutano na mvua kunyesha kubwa sana. Ndugu zangu, mvua ni Baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Naamini ndugu zetu walioshiriki nasi akina Abdallah Msesemele, Twaaha Nyange, Abdullah Mbanga na Sheikh Ame sahib watakumbuka tukio hili na namna lilivyoleta gumzo.

Hizi ndio Baraka za Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya kwa mkoa wa Shinyanga na ilivyoleta neema ya mvua pale mara tu baada ya kuadhimisha mkutano wake wa kwanza Jalsa Nau Mubaein mkoani kwetu, Baraka ambazo sio rahisi kuziona kwa jicho la kawaida. Ndugu zangu hii ikawa ni ishara kuwa kumbe Mwenyezi Mungu yu pamoja na jitihada hizi ndogo tunazozifanya kwa mkoa wa Shinyanga, japokuwa baadhi zaweza kubezwa kidogo. Mkutano huu wa mwanzo ambao ulishirikisha washiriki si zaidi ya 300 ukaisha kwa kiwango hicho, huku sisi waandaaji tukiwa n khofu na wasiwasi mkubwa sana juu ya je atatufikiriaje Amir sahib kwa mkutano huu kuwa kwenye mazingira haya. Kumbe Allah ametupokelea kwa hicho kidogo, na kutuonyesha kuwa neema kubwa na nyingi zitamiminika mkoani Shinyanga kwa ishara ya mvua kunyesha mwishoni, na kwamba jitihada hizo zitaendelezwa na kuwagiliwa na kuneemeshwa InshaAllah.

Tukiwa hatuna hili wala lile, tukaanza kuziona neema za Allah kwa jamaat yake zikizidi kupanuka kila uchwao, na hata kutuletea khofu kwamba tutawezaje kumudu kuwahudumia kiroho viumbe hawa wengi wa usukumani wanaokimbilia kuja kuungana na Jumuiya yake. Neema hizi zikawa ni nyingi, na wepesi kuonekana kimahubiri. Kumbe ni majibu ya ishara ya ile mvua kubwa iliyonyesha na kututeremkia sie viumbe wa Allah baada ya muda mrefu kutokuwa na mvua, baadhi yetu baada ya tukio lile la mvua basi tukabaini huu mkoa wa Shinyanga utakuja kupata Baraka kubwa na nyingi kijamaat na Allah ataumiminia kheri nyingi InshaAllah. Nakumbuka ndugu wengi waliotoka Jamaat mbalimbali vijijini wakanena yafuatayo:-

i) Yaani tumefanya mkutano, ile tunamaliza tu mvua ikaanza kwa mara ya kwanza kwa msimu mzima.

ii) Hii dini ya kweli maan siku zote mvua hainyeshi, leo imenyesha huenda dua zimepokelewa

iii) Kijiji cha Tinde yote kikaachwa na bumbuwazi kwa tukio kubwa la mvua

Licha ya kuona mkutano huu kama vile ulisuasua, lakini mbele ya Allah ilikuwa ni ishara kubwa sana kwetu. Kwamba, mikutano itakayofata basi itakuwa na fanaka na ufaulu mkubwa na matokeo chanya InshaAllah. Na kweli hicho ndicho kilikuja kutokea kwenye mikutano ya Jalsa nyinginezo zote zilizofuata mkoani Shinyanga. Tumeshuhudia mikutano iliyofuata ikihudhuriwa na Wakuu wa Mikoa ambao walishiriki siku nzima huku wakiambatana na kamati zao za Ulinzi na Usalama Mkoa, Wakuu wa Wilaya wakishiriki pi. Lakini kama haitoshi na ili tuzione neema zake Allah kwa kupitia Jalsa hiyo ya kwanza Shinyanga, Jalsa zilizofuata zimapata kuhudhuriwa na ndugu kadhaa kutoka nchi za mbali ka Sierra Leone kuja kushiriki Jalsa ya mkoa wa Shinyanga. Nitakuja kuelezea huko mbeleni juu ya ishara na miujiza ya Jalsa Nau Mubaein zote zilizofuata na zilikuwaje kwa kupitia ishara njema za Jalsa ya kwanza pale Tinde. Yafaa tutafakari nguvu zake Allah, nitakuja kuelezea

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Taasisi Ya Majlis Shura – Mashauriano

Kutoka uk. 12

kwa mujibu wa Amri ya Mwenyezi Mungu na mafundisho ya Mtume Mtukufu (saw), anashauriana na wanajumuiya katika nchi mbalimbali kuhusiana na hali zao na mambo yanayowahusu.

Shura ni Njia ya Kuvutia Rehema za Mwenyezi Mungu:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba mfano wa Mtume Mtukufu (saw) kuomba mashauriano kwa hakika ulikuwa wa kutuongoza sisi kwenye haki na kuimarisha umoja katika wafuasi wake. Imesimuliwa kwamba wakati Aya ya Kurani Tukufu kuhusu mashauriano ilipoteremshwa, Mtume Mtukufu (saw) alisema kwamba hiyo imeteremshwa kuwa rehema kwa wafuasi wake. Kwa hivyo, mtu anayeshauriana atapata baraka, na wale wasioshauriana hawawezi kuokolewa kutoka kwa fedheha. Hivyo, ingawa Mtume Mtukufu (saw) alikuwa anamtegemea Mwenyezi Mungu kikamilifu, hata hivyo alikuwa akishauriana na Masahaba wake ili atuongoze.

Njia Tatu za Mashauriano za Mtume Mtukufu (saw) na Makhalifa Walioongoka (ra):

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba kwa kuzingatia hili, tunapaswa kushukuru juu ya neema ya taasisi ya Majlis-e-Shura na kuiheshimu sana. Kuhusiana na namna Mtume Mtukufu (saw) alivyoshauriana, tunakuta kuna aina tatu za mashauriano; aina moja ilikuwa kwamba wakati ushauri ulipohitajika juu ya jambo fulani, tangazo lilikuwa likitolewa ili watu wakusanyike. Kisha Mtume Mtukufu (saw) alikuwa akishauriana na watu kuhusiana na jambo hilo, kisha alikuwa akitoa uamuzi wake. Ingawa watu wote walikusanyika, viongozi na wakuu wa makabila mbalimbali ndio walioruhusiwa kuzungumza kama wawakilishi wa watu wao, na watu waliridhika kabisa na njia hiyo. Namna ya pili ilikuwa kwamba Mtume Mtukufu (saw) alikuwa akiwaita hasa wale ambao alifikiria kwamba walikuwa wanafaa zaidi kutoa mapendekezo juu ya jambo fulani. Namna ya tatu ilikuwa hii kwamba Mtume Mtukufu (saw) alipoona inafaa, basi alikuwa akiwaita watu mmoja baada ya mwingine kuomba ushauri kutoka kwao. Hizi pia zilikuwa ni njia zile zile zilizopitishwa na Makhalifa wake walioongoka (ra).

Jinsi Mtume Mtukufu (saw) Alivyokuwa Akiomba Ushauri:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba imesimuliwa kwamba hakuna mtu aliyekuwa akiomba ushauri zaidi ya Mtume Mtukufu (saw). Kwa mfano, ilipokuja suala la kumtuma Hadhrat Mu'adh bin Jabal (ra) kwenda Yemeni, Mtume Mtukufu (saw) alishauriana na watu mbalimbali, wakiwemo Hadhrat Abu Bakr (ra), Hazrat Umar (ra), Hazrat Uthman (ra), Hazrat Talha (ra), Hazrat Zubair (ra), na Masahaba wengine wengi. Hadhrat Abu Bakr (ra) alisema kwamba kama Mtume Mtukufu (saww) asingewauliza, wasingesema chochote. Mtume Mtukufu (saw) alisema kwamba katika mambo ambayo alikuwa hajapata wahyi, alikuwa kama wao. Katika suala hili, Mtume Mtukufu (saww) pia aliuliza maoni ya Hazrat Mu'adh (ra). Kwa hivyo, hii inadhihirisha unyenyekevu wa Mtume Mtukufu (saw) na mkazo mkubwa unaotakiwa kutiliwa juu ya mashauriano.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba Mtume Mtukufu (saw) pia alishauriana na Masahaba wake baada ya kuhamia Madina, wakati watu wa Makka walitaka kuharibu amani ya Waislamu. Baada ya kushauriana nao, Mtume Mtukufu (saw) aliondoka kuelekea Badr. Kwa hakika, wakati wa mashauriano haya, wakuu wa Ansari walionyesha uaminifu mkubwa na hata wakala kiapo, ambacho kilimfurahisha sana Mtume Mtukufu (saw). Alifanya hivyo siyo kwa sababu hiyo tu kwamba mwenendo wa wale ambao ushauri unatafutwa kwao utiliwe mkazo mkubwa, bali lazima wao wawe katika mstari wa mbele pia katika kutimiza uamuzi wowote unaotolewa kutokana na mashauriano hayo. Kwa hivyo, wajumbe wote wa Majlis-e-Shura lazima wazingatie kwamba wawe mbele katika kutekeleza uamuzi wowote unaofanywa na Khalifa wa Wakati huo. Ni pale tu watakapoweka mifano yao wenyewe ya kivitendo ndipo wanajumuiya wengine wote watakuwa tayari kutekeleza wajibu wao na watakuwa tayari kutoa dhabihu yoyote inayohitajika kwa ajili yake.

Majukumu ya Wajumbe wa Shura:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba wajumbe wa Shura lazima wakumbuke kwamba kila Mwahmadiyya ameahidi uaminifu kwa Ukhalifa, na hivyo, lazima watimize kiapo hiki kwa kiwango cha juu kabisa. Kama vile Khalifa anapaswa kutii amri ya kuomba ushauri na kuwa na moyo wa rehema, wale wanaoombwa ushauri nao wana jukumu la kufanya hivyo hivyo, na kutoa mapendekezo yao kwa nia safi kabisa. Wajumbe wa Shura wanapaswa kutafakari juu ya kiwango cha ucha-Mungu wao. Imesimuliwa kwamba Hadhrat Ali (ra) alisema kwamba ni wenye busara tu na wale waliolinda ibada zao ndio waombwe ushauri. Hiki ndicho kiwango kinachotakiwa kwa wajumbe. Kwa hakika, huu pia ni mwongozo kwa wale wanaowachagua wawakilishi wa Shura. Wanapaswa kuchagua wale wanaoonekana kuwa na uwezo wa kutoa ushauri mzuri na wamejitolea katika ibada zao. Wakati hii ndiyo itakuwa sababu ya kuchagua wakilishi, basi tofauti ya wazi itaonekana katika mapendekezo yanayotolewa.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba wakati wa kutoa mapendekezo na kutoa maoni, wajumbe wa Shura wasishawishiwe na mtu mwingine, wasifikirie urafiki wao wa kibinafsi katika maoni wanayotoa, na wala wasibadili maoni yao wenyewe kwa kuogopa kitu kingine chochote. Bali, wanapaswa kutoa maoni yao huku wakiweka ucha-Mungu mbele katika fikira zao. Wanapaswa kukumbuka kwamba Mwenyezi Mungu Anajua yale yaliyomo mioyoni mwao na pia matendo yao. Wanapaswa kuogopa jambo hili kwamba ikiwa hawatachukua njia za kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu, basi wanaweza kupata hasira Yake.

Kupokea Baraka za Mwenyezi Mungu:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kuwa katika nchi ambazo Shura tayari imeshafanyika, wajumbe wanapaswa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuapa kuonyesha mifano yao ya vitendo huku wakizingatia hali zao za kiroho na kivitendo. Wanapaswa kufuata maamuzi yaliyotolewa kwa ucha-Mungu na pia kuhakikisha utimizo wake. Watakapofanya hivyo ndivyo wataweza kupokea baraka za Mwenyezi Mungu na maamuzi yaliyotolewa pia yatabarikiwa. Hili lisipofanyika, basi maamuzi yanayofanywa yanaweza kusababisha uharibifu au hata kuvuruga amani. Kwa hivyo, ili kuzuia hili, lazima tujichambue kila wakati.

Majlis-e-Shura ni kama Msaidizi wa Khalifatul Masih:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba mapendekezo yaliyotolewa yanatumwa kwa Khalifa wa Wakati huo. Kwa hakika, Shura inaitwa tu kwa maelekezo ya Khalifa wa Zama. Kwa hivyo, Majlis-e-Shura hufanya kama msaidizi wa Ukhalifa. Baada ya mfumo wa Ukhalifa, Majlis-e-Shura inashikilia umuhimu uliotukuka. Mjumbe wa Shura anashikilia nafasi hiyo kwa muda wa mwaka mmoja na wanapaswa kuelewa umuhimu na uzito wa nafasi hii. Ajenda ya Shura na mapendekezo yanayotolewa yanampa Khalifa wa Wakati ufahamu wa masuala yaliyopo katika nchi mbalimbali. Mapendekezo yanayotolewa wakati mwingine hayajumuishi namna kamili ambayo tatizo linaweza kutatuliwa, ambapo Khalifa wa Wakati anajumuisha vipengele tofauti ambavyo pengine havikuwa katika mtazamo wa wajumbe wa Shura. Idhini yoyote inayopokelewa inapaswa kutekelezwa na kila mwanachama wa Shura. Ni katika kufanya tu ili tuweze kuwa wasaidizi wa kweli katika utume wa Masihi Aliyeahidiwa(as).

Kutetea Utakatifu wa Shura:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba wakati mwingine wakati wa kutoa maoni, baadhi ya watu hupatwa na jazba zaidi na kusema kwa namna isiyostahiki utakatifu wa Shura. Kwa hiyo, badala ya kuonyesha jazba za kutoa hotuba kali, wanapaswa kutoa maoni yao kwa utulivu na kwa njia inayofaa. Wakati mwingine, Amir ambaye anaongoza kikao anaweza kufikiria kwamba mtu anayetoa maoni yake anazungumza dhidi yao au kamati yao ya Amila na kisha kuwazuia kuzungumza. Hata hivyo, Amir anapaswa kuwa mwenye busara, na azingatie kwamba mtu anayetoa maoni yake anafanya hivyo kutokana na uchungu kwa ajili ya Jumuiya. Vilevile, mambo kama vile bajeti yanapojadiliwa, kunaweza kuwa na nyakati ambapo watu wana maoni makali sana. Badala ya kuruhusu hisia zitawale, kila mtu anapaswa kutulia na kusikiliza mapendekezo ya mwenzake akijua kwamba kila mtu anatafuta manufaa ya Jumuiya kwa jumla. Ikumbukwe *kila mara kwamba wakiwa ni wajumbe wa Shura, wamechaguliwa kuwa wawakilishi* na hivyo kamwe kitu chochote kisiwe cha kibinafsi au cha ubishi. Baada ya kuchaguliwa kuwa wawakilishi, ikiwa wajumbe hawako katika kiwango cha ucha-Mungu kinachohitajika, basi lazima waendelee kuomba msamaha na kujitahidi kuboresha hali zao. Ni lazima wawe wasaidizi wa Khalifa wa Wakati, na lazima wahakikishe kwamba maamuzi aliyoyafanya Khalifa wa Wakati yanatekelezwa vizuri na vile yalivyotolewa.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

SHAWAL-DHUL'QAD.1444AH | JUNI 2023 | ZAHOOR 1402 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Abu Huraira*ra* anasimulia kwamba: Nilimsikia Mtume*saw* akisema: Abu Huraira wallahi mimi naomba msamaha kwa Allah kutubia kwake kwa siku moja zaidi ya mara sabini (**Bukhari**).

Taasisi Ya Majlis Shura – Mashauriano

Baada Ya Kusoma Tashahhud, Taawwudh na Surah Al-Fatiha Hadhrat Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano (atba) alisoma Aya ifuatayo ya Kurani Tukufu:

فَبِمَا رَحْمَةٍ مِّنَ اللّٰهِ لِنْتَ لَهُمْ ۚ وَلَوْ كُنْتَ فَظًّا غَلِيْظَ الْقَلْبِ لَانْفَضُّوْا مِنْ حَوْلِكَ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ وَشَاوِرْهُمْ فِي الْأَمْرِ ۚ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللّٰهِ ۚ إِنَّ اللّٰهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِيْنَ۔

(Surah Aali Imran 3: 160)

"Basi kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu umekuwa laini kwao; na kama ungekuwa mkali na mwenye moyo mgumu, bila shaka wangalikukimbia. Basi uwasamehe na uwaombee msamaha na ushauriane nao katika mambo (yaliyo muhimu); na ufungapo nia, basi umtegemee Mwenyezi Mungu; hakika Mwenyezi Mungu Anawapenda wamtegemeao."

Umuhimu wa Taasisi ya Shura:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba siku hizi nchi mbalimbali zinafanya Majlis-e-Shura (mkutano wa kikundi cha mashauriano). Hudhur (atba) alisema kwamba ingawa amezungumza kuhusu umuhimu wa Shura na wajibu wa wajumbe wake, hata hivyo kwa vile imepita miaka michache, Hudhur (atba) alisema kwamba aliona inafaa kuzungumzia suala hilo tena kama ukumbusho kwa kuzingatia amri za Mwenyezi Mungu, Mtume Mtukufu (saw) na mafundisho ya Jumuiya.



*Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tano*atba *akihutubia waumini katika Masjid Mubarak, Uingereza siku ya Tarehe 12 Mei 2023, kuhusu Taasisi ya Majlis Shura – Mashauriano.*

Hudhur (atba) alisema kwamba hata katika nchi ambazo Shura tayari imeshafanyika, wajumbe bado wanaweza kufaidika na ushauri huu, kwa sababu majukumu yao yanaendelea baada ya Khalifa wa Zama kuridhia mapendekezo yao ili kuhakikisha yanatekelezwa.

Inapaswa Kumtegemea Mwenyezi Mungu Kikamilifu:

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba ataangazia vipengele fulani katika mwanga wa Aya aliyoisoma hapo mwanzo pamoja na mfano wa Mtume Mtukufu (saw). Katika Aya hiyo, Mwenyezi Mungu Anashuhudia ukweli kwamba Mtume Mtukufu (saw) alikuwa na huruma mno kwa watu wake. Aya pia inaeleza kwamba wale waliopaswa kutekeleza kazi hiyo hiyo, hasa mtumishi wake wa kweli atakayekuja katika siku za mwisho alipaswa kuonyesha rehema na huruma ile ile. Mwenyezi Mungu Anasema badala ya huruma, ikiwa hasira na ukali zingeonyeshwa, basi watu wangekimbia, ndiyo maana amri ya kusamehe na kumwomba Mwenyezi Mungu msamaha imetolewa. Vile vile, amri ya mashauriano pia imetolewa. Hivyo ndivyo Majlis-e-Shura inavyofanywa, lakini kama jina linavyoonyesha, mkutano huu unafanywa kwa kutoa ushauri, siyo kufanya maamuzi. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu Anasema kwamba baada ya kushauriana, uamuzi unapofanywa, basi Mwenyezi Mungu Anapaswa kutegemewa kikamilifu.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba mfano kamili wa kumtegemea Mwenyezi Mungu ni wa Mtume Mtukufu (saw). Ingawa Mtume Mtukufu (saw) alipokea wahyi wa Mwenyezi Mungu ili kufafanua mambo mbalimbali yaliyohitaji ufafanuzi, Mtume Mtukufu (saw) pia alikuwa akishauriana na Masahaba wake kuhusiana na mambo ambayo wahyi wa Mwenyezi Mungu ulikuwa bado haujapokelewa. Hilo linatuonyesha jinsi wenye nyadhifa wanavyopaswa kuwatendea wanajumuiya, na jinsi tunavyopaswa kushauriana. Tuna bahati kubwa kwamba Mwenyezi Mungu Aliijaalia Jumuiya ya Ahmadiyya baraka ya Ukhalifa. Kwa hivyo, Khalifa wa Wakati huo,

Endelea uk.11

SIRI
YA
UHAKIKA

Na
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad*as* wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi
Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
Tanzania

Kitabu hiki kilichapishwa mnamo 1898. Katika kitabu hiki, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad*as* wa Qadian, Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi, ametoa mwanga historia ya kweli ya maisha ya Yesu Kristo na kueleza na ushahidi wa kihistoria kwamba Isa bin Mariamu. Alikuwa ameokoka kusulubishwa na kuhamia India ambapo alikufa akiwa na umri wa miaka 120 na kuzikwa katika maeneo ya Khanyar ya Srinagar, Kashmir. Mchoro wa kaburi lake huko Srinagar pia umetolewa katika kitabu.

Nusu ya baadaye ya kitabu imetolewa kwa kiasi kikubwa kukanusha ukosoaji uliofanywa na Maulawi Muhammad Husain kuhusu lugha ya ufunuo wa Kiarabu wa Masihi Aliyeahidiwa.

Masihi Aliyeahidiwa amejibu pingamizi hilo kwa hoja za kimantiki na zenye mantiki zinazonukuu mifano kutoka kwenye Hadith za Mtukufu Mtume saw. Rehema na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na washairi mashuhuri wa Arabuni, na wakauthibitisha uungu huo ufunuo ulikuwa zaidi ya lawama na ulitimiza yote mahitaji ya sarufi ya Kiarabu.

Nakala hii itapatikana kwa Sh. 2,300/=

Je, Wajua?

Je wajua kuwa mwaka 2018 NASA (shirika la anga la marekani) lilituma combo kilicholengwa kufika katika jua. Chombo hicho kinaweza kuhimili joto la 2,500 F (1,377 C). Tarehe April 28, 2021, chombo hicho kiitwacho parker space probe kilifika katika anga ya jua na kupiga picha. Mpaka leo hii chombo hicho kimezunguka jua mara kadhaa na kinaendelea kukusanya taarifa mbalimbali kuhusu jua.

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie
mapenziyamungu36@gmail.com